



## **TAARIFA KWA UMMA**

**(Iliyorekebishwa)**

### **USIMAMIZI KWA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA**

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 mnamo tarehe 16 Novemba 2018, ili kutekeleza matakwa ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017. Kifungu cha 12 cha Sheria hiyo kimeipa mamlaka Benki Kuu ya Tanzania Kusajili, Kusimamia na Kudhibiti biashara ya huduma ndogo za Fedha Tanzania Bara. Vile vile, Sheria imetoa tafsiri juu ya “huduma ndogo za fedha” kuwa ni biashara inayojumuisha kupokea fedha, kama amana au riba kutokana na amana au mkopo na kuikopesha kwa wanachama au wateja; kupokea amana na kutoa mikopo au huduma ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo, kaya au mtu mmoja mmoja; kutoa huduma za mikopo midogo, akiba ndogo, bima ndogo, huduma ndogo za karadha, pensheni ndogo na mikopo midogo ya nyumba; huduma za kutuma fedha na malipo, ikijumuisha huduma ndogo za fedha kwa njia ya mtandao; kutoa elimu ya fedha; na huduma nyingine zinazofanana na hizi kama zitakavyoainishwa kwenye kanuni za Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018.

Kifungu cha 16 cha Sheria hiyo kimetoa katazo kwa mtu au taasisi yoyote kufanya biashara ya kutoa huduma ndogo za fedha bila kuwa na leseni iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, Sheria imeweka adhabu itakayotolewa kwa mtu au taasisi yoyote itakayokiuka matakwa ya Kifungu cha 16.

Benki Kuu ya Tanzania iko katika hatua ya kuandaa Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa huduma ndogo za fedha kulingana na madaraja tofauti yaliyoainishwa kwenye Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018. Aidha, mtu au taasisi yoyote inayohitaji kufanya au kuendelea kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha itahitajika kuomba upya leseni ya Benki Kuu ya Tanzania, pamoja na kukidhi matakwa yote kama yatakavyoainishwa katika kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa huduma ndogo za fedha ambazo zitachapishwa kwenye Gazeti la Serikali mara zitakapokuwa zimekamilika.

Hivyo basi, Benki Kuu ya Tanzania inawataka watu na taasisi zote zinazofanya biashara ya huduma ndogo za fedha (isipokuwa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo – SACCOS) kuwasilisha taarifa zilizoainishwa hapo chini. Taarifa hizo zinatakiwa kufika Benki Kuu ya Tanzania tarehe **31 Januari 2019**:

- a) Cheti cha Uandikishwaji (Certificate of Incorporation)
- b) Leseni ya Biashara iliyotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)
- c) Eneo/Sehemu ya Biashara na taarifa za anuani:
  - (i) Anuani ya Eneo (Mtaa/Kijiji, Wilaya na Mkoa)
  - (ii) Namba ya Simu
  - (iii) Anuani ya barua pepe
- d) Orodha ya wamiliki, Bodi ya Wakurugenzi, Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Uraia wao.
- e) Aina ya huduma ndogo za fedha zitolewazo.
- f) Taarifa kama mahesabu ya taasisi/biashara yamekaguliwa au hayajakaguliwa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.
- g) Maelezo ya mfumo unaotumika kutunza taarifa za fedha, mawasiliano na teknolojia.
- h) Taarifa ya fedha, ikionesha:
  - (i) Jumla ya mali (Assets)
  - (ii) Jumla ya madeni (Liabilities); na
  - (iii) Jumla ya Fedha za Wanahisa (Owners' Equity)

Taarifa zilizoordheshwa hapo juu zitumwe kwa Mkurugenzi wa Usimamizi wa Taasisi za Fedha, Benki Kuu ya Tanzania-Makao Makuu, Ghorofa ya 6 Mnara wa Kaskazini, S.L.P. 2939, Dar es Salaam au baruapepe kwa: [vctarimu@bot.go.tz](mailto:vctarimu@bot.go.tz); [nfmongateko@bot.go.tz](mailto:nfmongateko@bot.go.tz); na [dasasya@bot.go.tz](mailto:dasasya@bot.go.tz)

**BENKI KUU YA TANZANIA**

05 JANUARI 2019